Ijumaa04/Rabiul Awwal/1428 H =23/03/2007 AD,Pongwe-Tanga,Tanzania.makala namba 12.

# HII NDIYO DAAWA YETU

# JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

## UKWELI KUHUSU TOBA YA IBNU SINA (AVICENNA)

Amesema al Hafidh Ibin Hajar(852h);
فقطع علماء زمانه ومن بعدهم من الأئمة ممن يعتبر قولهم أصولا وفروعا بكفره ....
Wamepitisha hukumu wanawachuoni wa zama zake,na waliofuatia baada yao, miongoni mwa wanawachuoni wanaotegemewa kauli zao katika mambo ya misingi na matawi juu ya ukafiri wake(Ibnu Sina)!!!!
Tazama lisaanul mizani juz 1,uk293.

MUANDISHI;

AL AKH ABUL FADH'LI QASSIM MAFUTA QASSIM.

بسم الله الرحمن الرحيم

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote,na shukrani zote.
Ni zako wewe sifa njema vile zinavyo lingana na utukufu wako,na ukubwa wako,ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike,na pale unaporidhika, na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu,Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake,na maswahaba zake wote,na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Ndugu muislamu! Napenda ufahamu kwamba ukweli siku zote utabaki kuwa ni ukweli hata kama utapewa jina baya,na kutupwa kwa maneno ya kinyaa na kejeli, na urongo utaendelea kuwa ni urongo,hata kama utapewa hadhi na heshima,na kupambwa kwa maneno matamu.

Katika makala yetu namba 10,nilizungumzia ubaya wa kuwaadhimisha na kuwaenzi watu wa Bid'a, kwa mujibu wa misingi ya Ahli Sunna wal jamaa,na nikamlenga moja kwa moja Imamul mul'hidina Ibnu Sina,na nikazitaja kauli za baadhi ya wanawachuoni wa Ahli Sunna juu ya itikadi zake chafu,na namna walivyo muhukumu na kumtoa nje ya Uislamu,jambo ambalo halikuwafurahisha watetezi wake,na hatimaye kufanya jaribio la kumtetea bwana huyu kwa ukali kabisa,na maneno mengi yaliyo jaa upotoshaji wa haki kama utakavyoona ndugu msomaji katika makala yetu hii-Inshaallah-.

Ilikuwa ni matarajio yangu kwamba wahusika wa jambo hili watatanabahi na makosa waliyo yafanya, kisha kujirekebisha au kama wanayo majibu basi yawe majibu ya kielimu !!

Lakini mambo yalikuwa kinyume cha hivyo,bali yalitoka majibu ambayo yamejaa kejeli ! ubabaishaji,na kuwatia watu mchanga wa macho,ili kuwaonyesha watu kwamba amejibu!!

Na natija ya majibu hayo ni kwamba hakuna vibaya kumuadhimisha Mul'hid huyo!
Wengi ambao hawakusoma,na hata wale ambao wamesoma lakini wana upeo mdogo wa kutafiti mambo ya kielimu walighurika na majibu hayo.
Hivyo basi tumeonelea katika makala hii tuweke sawa mambo,na kuwabainishia watu kwamba hakuna majibu ya kielimu yaliyotolewa,bali ilikuwa ni vunga bwege tu !!

## 1-Ni nini hukumu ya kumkufurisha Muislamu?

Kwa mujibu wa misingi ya Ah'li Sunna wal Jama'a haifai kumuita muislamu kuwa ni kafiri,bila ya kutumika vigezo vya kisheria,na jambo hili amelikemea sana Bwana Mtume-rehma na amani zimfikie-aliposema;

( إذا قال الرجل لأخيه يا كافر فقد باء به أحدهما)

"Atakaye sema mtu kumwambia ndugu yake yaa kafir! basi litamrudia jambo hilo mmoja wao".

Tazama sahihi Bukhari hadithi namba; 5752.

Amesema Sheikh al Fawzan;

"ليس من حق كل أحد أن يطلق التكفير أو يتكلم بالتكفير على الجماعات،أو على الأفراد. التكفير له ضوابط فمن يرتكب ناقضاً من نواقض الإسلام فإنه يحكم بكفره".

"Siyo haki kwa kila mtu kutoa hukumu ya ukafiri,au kukufurisha makundi au mtu (mmoja mmoja). Kukufurisha kuna vigezo vyake, yule atakaye tenda kichanguzi miongoni mwa vichanguzi vya uislamu basi atahukumiwa ukafiri'.

Tazama al muntaqa min fatawih juz 1 uk 112.

Na siku zote maulamaa wa Ahli Sunna wanawatahadharisha watu juu ya suala hili,na kuwabainishia hatari zake.

Hivyo basi haifai kumuita muislamu kafiri bila ya vigezo vya kisheria, kwasababu jambo hili ni la hatari mno, hivyo basi tunasema;

kwa mujibu ya itikadi ya Ahli sunna wal jamaa ni makosa kumkufurisha asiyekuwa kafiri,pia ifahamike kwamba;

Ni katika vitenguzi vya uislamu kutomkufurisha kafiri.

Pia nataka ifahamike kwamba suala hili nyeti ni kazi ya maulamaa wa kiislamu, wao ndiyo walio na wadhifa wa kutoa hukumu juu ya suala hili zito, na siyo kila mtu ana nafasi ya kumuhukumu mtu. Nasisi –walillahil hamdu- tunafuata utaratibu huu.

## 2- Je ni kweli Ibnu Sina alikufuru?

Je ni kweli kwamba Ibnu Sina alikufuru? Na kama alikufuru je ni mambo gani hayo yaliyomtia katika ukafiri?

amesema Imamu Ibnu Kathir;

قد حصر الغزالي كلامه في مقاصد الفلاسفة ثم رد عليه في تهافت الفلاسفة في عشرين مجلسا له كفره في ثلاث منها

– وهي قوله يقدم العالم

– وعدم المعاد الجثماني

– وان الله لا يعلم الجزئيات

–وبدعه في البواقي

"Na al Ghazaly ameyadhibiti maneno yake katika (kitabu chake) Maqasidul falasifa na kumrudi katika kitabu Tahafutil falasifa katika maj'lis ishirini,na kumkufurisha katika majlisi tatu,katika hizo ni;
-kauli yake kwamba ulimwengu ni wakale (na hauna mwanzo)
-kupinga kufufuliwa viwiliwili (siku ya Qiyama)!!
-na kwamba Allah s.w.t. hayajui mambo kwa juz'iyyaati (upambanuzi)!!
-na akamtia katika bid'a kwa mambo yaliyo bakia".

Tazama al bidayatu wannihayat juzuu ya 12/ukurasa 489.

Amesema al Qadhy shihabud- Din Ibrahim bin Abdillahi maarufu kwa jina la Ibin Abid- Dam;

: " واتفق العلماء على أن ابن سينا كان يقول بقدم العالم ونفى المعاد الجسماني وأثبت المعاد النفساني .

ونقل عنه أنه قال : إن الله تعالى لا يعلم الجزئيات بعلمٍ جزئي وإنما يعلمها بعلمٍ كليٍّ

. وقطع علماء زمانه ومن بعده الأئمة المعتبرة أقوالهم أصولاً وفروعاً من الحق بكفره وبكفر أبي نصرٍ الفارابي

" بهذه المسائل الثلاث واعتقاده فيها بما يخالف اعتقاد المسلمين

**الوافي في الوفيات 1/1755**

""Na wameafikiana maulamaa kwamba Ibnu Sina alikuwa akisema;

Ulimwengu ni wa kale(hauna mwanzo),
Anakana kufufuliwa viwiliwili,
Na kwamba Allah hayajui mambo kwa elimu ya upambanuzi,bali anayajua kwa elimu ya ujumla,
(hivyo basi) wakapitisha hukumu maulamaa wa zama zake na waliokuja baada yake,- maulamaa ambao huzingatiwa kauli zao katika usuuli (itikadi) na matawi katika mambo ya haki-juu ya ukafiri na ukafiri wa (mwalimu wake) al Faraaby kwasababu ya haya mambo matatu,na itikadi yake katika yale anayo hitalifiana na waislamu"!!
Tazama al waafy fil wafayaat 1/1755.
Katika maneno haya tunapata faida zifuatazo;

a)Ibnu Sina amekufurishwa na maulamaa wa zama zake,na hata wale walio kuja baada yake!miongoni mwao ni Imamu al Ghazaaly.

b)sababu zilizo mpelekea kuingia katika ukafiri ni;
-kauli yake ya kwamba ulimwengu ni wa kale,na hauna mwanzo!
-kumnasibishia Allah ujinga!
-anapinga kufufuliwa kwa viwiliwili siku ya Qiyama !

Na bila shaka kiislamu mwenye itikadi hizi si muislamu,na wala hana fadhila yoyote mbele ya Allah,wala mbele za viumbe.

## 3-Je Ibnu Sina aliwahi kuwa mtu wa Sunna?

Ukweli ni kwamba Ibnu Sina hakuwahi kuonja ladha ya msimamo wa Sunna bali alikuwa yeye na baba yake,na familia yake kwa ujumla ni katika Qaraamitwa (1).

Amesema Ibnul Qayyim;

وكان ابن سينا كما أخبر عن نفسه قال :
أنا وأبي من أهل دعوة الحاكم فكان من القرامطة الباطنية الذين لا يؤمنون بمبدأ ولا معاد ولا رب خالق ولا رسول مبعوث جاء من عند الله تعالى
وكان هؤلاء زنادقة يتسترون بالرفض ويبطنون الإلحاد المحض ...إغاثة اللهفان 266/2.

"Na alikuwa Ibnu Sina kama alivyojielezea mwenyewe, amesema;
Nilikuwa mimi na baba yangu ni wafuasi wa da'awa ya Hakim,naye alikuwa ni katika Qaraamitah baatiniyyah, ambao hawaamini mwanzo (wa kuumbwa vitu) wala kufufuliwa, wala hawamuamini mola muumba wala Mtume aliyekuja kutoka kwa Allah.
Na wazandiki hawa walikuwa wakijificha (nyuma) ya Ushia, na walikuwa wakiuficha ukafiri wao " !

Tazama kitabu Ighaathatul lah'fan cha Ibnul Qayyim,juz 2, uk;266.

Huyo ndiye Ibnu Sina wenu,mshia Qaramitwa yeye na baba yake!
Bila shaka wale ambao wanaisoma historia ya kiislamu wanafahamu uovu na ukafiri uliyofanywa na Qaramitwa katika Umma wa kiislamu!

(1)Qaramitwa ni pote la kishia baatiniyya,ambao ni wafuasi wa Hamdani bin Ash'ath, moja kati ya itikadi zao ni kupinga kufufuliwa watu siku ya Qiyama,na kuhalalisha ufuska n,k. tazama al mausuatul muyassara juz 1 uk 378-382.

Moja kati ya uovu wao ni kuwauwa waislamu katika nyumba tukufu ya Allah (al Ka'aba) na kulipora jiwe jeusi (Hajarul as'wad) na kukaa nalo takriban miaka ishirini na tatu!!

Kwahiyo basi hata kama Ibnu Sina atapona na ukafiri wa mambo hayo matatu,bado atakuwa anakabiliwa na bid'a na kufru ya Uqaramitwa!
Je bado kwenu ni mtu wa kuadhimishwa?

Na je hamjui kwamba haifai kuwaadhimisha watu wazushi?
Amesema Fudhail Ibnu I'yadh;

(( من عظم صاحب بدعة فقد أعان على هدم الإسلام...))

شرح السنة للبربهاري ص 139.

"Mwenye kumuadhimisha mtu wa bid'a atakuwa amesaidia juu ya kuuvunja uislamu".
Kitabu Shar'hu Sunna cha al Bar'bahary uk 139.

## Fatawa za maulamaa juu ya ukafiri wa Ibn Sina

Hapa tunalazimika kutaja tena kauli na fatawa za maulamaa juu ya Ibn Sina.
1- Amesema Imamu ad Dhah'by;

الحسين بن عبد الله بن سيناء أبو علي الرئيس:
ما أعلمه روى شيئا من العلم ولو روى لما حلت الرواية عنه لأنه فلسفي النحلة ضال لا رضي الله عنه انتهى

Al Hussein bin Abdillahi Ibin Sina,Abu Ally ar Raisy;
Sijui kama amepokea kitu chochote katika elimu-za hadithi- na hata kama angepokea isingekuwa halali kupokea kutoka kwake,kwasababu yeye alikua ni mtu wa falsafa,na ni mpotevu,na ALLAH ASIWE RADHI NAYE!!!!
Lisanul mizani juz 1,uk291.

2-Na amesema al Hafidh Ibin Hajar;

فقطع علماء زمانه ومن بعدهم من الأئمة ممن يعتبر قولهم أصولا وفروعا بكفره ....

Wamepitisha hukumu wanawachuoni wa zama zake,na waliofuatia baada yao, miongoni mwa wanawachuoni wanaotegemewa kauli zao katika mambo ya misingi na matawi juu ya ukafiri wake!!!!
Tazama lisaanul mizani juz 1,uk293.

3-Na amesema al Imamu Ibin Kathir;

وقد أطلق الغزالي وغيره القول بتكفير بن سيناء

Na ametoa hukumu Imamu al Ghazaly na wengineo juu ya ukafiri wa Ibin Sina…!!!
Tazama al bidayatu wannihayat juz12,uk489.
Na amesema Imamu Ibnul Qayyim;

واتخذ للملاحدة مدارس ورام جعل إشارات إمام الملحدين ابن سينا مكان القرآن .....
وبالجملة فكان هذا الملحد هو وأتباعه من الملحدين الكافرين بالله وملائكته وكتبه ورسله واليوم الآخر...

Na akawajengea Mul'hidina madarsa,na akataka kuziweka ishara za imamu wa mul'hidina Ibin Sina mahali pa Qur'an…..kwa ujumla –ni kwamba –alikua Mul'hidi huyu na wafuasi wake ni katika Mul'hidina wenye kumkufuru Mwenyezi Mungu,na Malaika wake,na Vitabu vyake,na Mitume yake,na Siku ya mwisho….)).

tazama Ighaathatul lah'fani juzuu ya 2,ukurasa 531-535.

Na amesema Sheikhul Islami Ibin Taymiyyah;

....وهذه طريقة الفارابى وابن سينا لكن ابن سينا الإيمان من بعض الوجوه وإن لم يكن مؤمناً

…..na hii ndiyo njia ya al Faraby,na Ibin Sina,lakini Ibin Sina yuko karibu zaidi katika imani kuliko baadhi ya njia,ijapokuwa si muislamu..!!!!!
Maj'muu fatawa 12/22.

Amesema tena Ibin Taymiyyah;

كان فقهاء بخارى يقولون فى ابن سينا كان كافرا ذكيا...40/9 مجموع الفتاوى.

Walikuwa wanawachuoni wa Bukhara wanasema kuhusu Ibin SINA kwamba; alikuwa KAFIRI mwerevu!!
Maj'muu fatawa 9/40.

**Aliulizwa Sheikh Abdul Aziz Ar Rajihi juu ya wale wasio wakufurisha wenye itikadi kama za Ibn Sina (AVICENNA)**

SWALI; kwa kuzingatia sharia ya kukufurisha (TAKFIR) Yeyote yule ambaye hatowachukulia washirikina kuwa ni makafiri, kama vile IBN SINA, Na akaja mtu kusema "Mimi sioni kuwa IBN SINAA ni kafiri,

Kwangu mimi ni muislamu" Je, mtu huyu atakuwa amejiingiza kwenye ukafiri?

JAWABU; ikiwa kama hamuelewi yeye (IBN SINA) na vilevile hafahamu hali yake (itikadi yake) basi hatochukuliwa kuwa yeye ni kafiri mpaka kwanza afahamishwe mambo yake yaani asimamishiwe hojja. Ama yule ambae anajua kuwa huyu Ibn Sinaa ni kafiri, na kwamba yupo kinyume na itikadi sahihi na akawa bado hamchukulii kuwa yeye ni kafiri basi mtu huyo ataangukia katika moja ya vitenguzi hivi vya UISLAM, Yeyote ambae hatomkufurisha kafiri, Au akawa na shaka juu ya ukafiri wake, Au akasawazisha iman zao za ukafiri kuwa ni sahihi, basi mtu huyo atakuwa amekufuru yeye!

Tazama fatawa hiyo katika web hii; http//www.salafitalk.net

## 4-Je baada ya ukafiri wake aliwahi kuleta toba?

Nilitaja katika makala yangu namba 10 baadhi ya maneno ya ulamaa wa Ah'li Sunna juu ya toba ya mtu huyu,na kuishiria kwamba toba yake haikutimiza masharti ya kukubaliwa, na ndiyo nikahoji na ninaendelea kuhoji kama ifuatvyo;

kwanini maulamaa waliokuja baada yake hawakuizingatia toba yake, na wakawa bado wanaendelea kumpa hukumu ya ukafiri na hali ya kuwa ametubu?!!

Mbona Ibnul Qayyim aliyekuja baada yake kwa miaka 323 anamuita; Mul'hid !Imamul Mul'hidina al kaafirina!?
Mara Sheikhul Islami Ibnu Taymiyya naye anamuita
Mzandiki ?! Mul'hidi?! mara ananukulu kauli za maulamaa zinazo mkufurisha bila ya kuzitolea maelezo wala kuzipinga?!

Kwanini Imamu ad Dhah'by aseme; si halali kupokea riwaya zake? Mara aseme; Allah asiwe radhi naye?!

Je wamefanya hivyo kwa chuki zao binafsi au ndiyo hali halisi ilivyo? na kuwa hiyo ndiyo hukumu yake stahiki ?
Na kuwa wamefanya hivyo kwasababu ya kutokamilika masharti ya toba?
Bila shaka wahusika wanalazimika kulijibu swali hili kielimu, badala ya kutumia ujanja,na kuwavunga watu wasio soma.

Amesema Sheikh Ibnu Uthaimin Allah amrehemu alipokuwa akiitafsiri aya ya 160,ya Suratul Baqarah;

(أن من تاب عن بدعة وضلالة فإنه يجب أن يبيِّنَ هذه البدعة والضلالة ،وأنه رجع عنه وتاب إلى الله منها وهذه كانت طريقة أهل العلم..)

"Mwenye kutubia kuacha bid'a,na upotevu wowote ule,ni wajibu juu yake kubainisha bid'a hiyo na upotevu huo na kwamba yeye amerejea na ametubu kwa Allah,na huo ndiyo utaratibu wa wanawachuoni (wa Sunna)

Swali,ni wapi Ibnu Sina ametubia kwa masharti hayo? na ni wapi amezibainisha bid'a zake hizo?
Wapi Ibnu Sina ameukana upotovu wake na kuupinga?
Ama kusema kwamba;Ibnu Sina alioga, akaswali, akatubia, akawaacha huru watumwa,akawa anakhitimisha Qur'an kila baada ya siku tatu! na amekufa siku ya ijumaa!

Hayo yote bado hayajakua ni ushahidi wa kwamba amezikana bid'a zake, na kuupinga upotovu wake na kufru zake,na hakuna mwanawachuoni yoyote anayesema kwamba Ibnu Sina alikufuru kwasababu alikua haogi,au hatoi sadaka,au haswali,au kwasababu ya kutosoma Qur'an, na kutowaacha huru watumwa,bali mambo yaliyo mkufurisha ni yale tuliyo yataja,na hakuna moja kati ya hayo alilolibainisha kuwa ni uopotovu au kulikana.
Ni sawasawa na mtu amdhulumu mwenzake haki yake, halafu kabla ya kufa kwake atubie kwa kupiga mswaki? Halafu useme si tayari ameshatubia ! na kuanza kutaja dalili,na ushahidi wa fadhila za kupiga mswaki !
Bila shaka utawashangaza walimwengu wachilia mbali wasomi !
Huyo ndiye Ibnu Sina ambaye mnasema kuwa ametubia, yeye ametetea bid'a na kufru katika maisha yake na kuuficha ukweli.
Na maulamaa wamemsimamishia hoja kwa mijadala,na vitabu lakini aliendelea na upotovu wake na kuutetea, kisha alipokaribia kufa badala ya kuibainisha kufru yake na kuipinga, twaambiwa eti alioga! Akawaacha huru watumwa n.k !
Je hayo ndiyo yaliyo mkufurisha?
Tunatarajia kuwa wafuasi wake watalijibu swali hili bila ya kuleta ubabaishaji kama ilivyo kawaida yao kubabaisha.

## 5- Man'haji ya Ah'li Sunna juu ya toba ya mzushi

Itakuwa ni vyema katika sehemu hii nikinukulu baadhi ya kauli za ulamaa wa Sunna juu ya suala zima la toba ya mzushi au kafiri aliyekuwa akilingania bid'a au upotofu.

Kwa ufupi ni kwamba; katika misingi ya Ah'li Sunna waljamaa mtu akikufuru au akitetea bid'a,au akificha haki, anapoleta toba,basi ni lazima masharti matatu yatimie;

Amesema Sheikh Ibin Uthaymin alipokuwa akiifasiri aya isemayo;

{إِلاَّ الَّذِينَ تَابُواْ وَأَصْلَحُواْ وَبَيَّنُواْ ........ }البقرة160

"Ila wale ambao wametubu,na wakatengeneza (amali zao) na wakabainisha(yale waliyo yaficha)…."160 al Baqarah,

akasema;

ذكرنا أن توبة أهل البدع –مثلاً-لاتكون إلاّ بالبيان والإصلاح لقوله تعالى :
{إِلاَّ الَّذِينَ تَابُواْ وَأَصْلَحُواْ وَبَيَّنُواْ ........ }البقرة160
ثلاثة شروط:
1- توبة الرجوع عما حصل بالكتمان.
2- إصلاح ما فسد بالكتمان.
3- بيان الحق غاية البيان. وبهذا تذهب سيئاتهم بحسناتهم.
ومن فوائد الآية الكريمة:
ويؤخذ منها أن من تاب عن بدعة وضلالة فإنه يجب أن يبيِّنَ هذه البدعة والضلالة ،وأنه رجع عنه وتاب إلى الله منها وهذه كانت طريقة أهل العلم....."

"tumetaja kwamba toba ya mzushi mathalani haitotimia ila kwa kubainisha na kutengeneza kwasababu ya kauli yake Allah isemayo;

*{Ila wale ambao wametubu,na wakatengeneza (amali zao) na wakabainisha (yale waliyo yaficha)…"*

Masharti matatu;
1-kutubia kwa kuyarudi yale yaliyo patikana kwasababu ya kuficha.
2-kuyatengeneza yale aliyo yaharibu.
3-kubainisha haki mwisho wa kubainisha na kwa mambo haya ndiyo mema yao yataondoa maovu yao.

Na katika faida za aya hii tukufu;

Tunachukua kutoka katika aya hii kwamba;
mwenye kutubia kuwacha bid'a na upotevu ni wajibu kwake kubainisha bid'a hiyo na upotofu huo (na abainishe) kwamba amerudi na ametubu kwa Allah,na hii ndiyo njia ya maulamaa.."
Tafsiri ya surat al Baqara aya ya 160, Ibnu Uthaymin.

Huo ndiyo msimamo wa Ahli Sunna juu ya toba ya mzushi  na wale wote wenye kulingania ukafiri na upotevu,haitoshi mtu kusema nimetubu au kusoma Qur'an, kuswali, kulia, kutoa sadaka, na kuacha huru watumwa! Haito zingatiwa toba yake mpaka atimize masharti hayo matatu.
Na bila shaka Ibnu Sina hakutimiza masharti hayo, badala yake twaambiwa kuwa kabla ya kufa alioga! Akaswali ! Akatoa sadaka!Akawacha huru watumwa! na akawa anahitimisha Qur'an kila baada ya siku tatu !
Swali; hatukatai hayo,je ametengeneza aliyoyaharibu?
Je amebainisha kwamba msimamo wake wa kikafiri aliokuwa nao kuwa ni batili?

Je amebainisha kwamba dunia ina mwanzo na si ya kale kama alivyo kuwa akiitakidi? na kutetea?

Je amebainisha kwamba Allah anayajua mambo kwa undani ? Na kwamba vile alivyo kuwa akiitakidi kwamba Allah hajui mambo kiundani ni batili?

Je amebainisha kwamba Allah atazifufua roho na viwiliwili? kinyume na itikadi yake potovu kwamba Allah atafufua roho tu?
Kama jawabu ndiyo,ni wapi kayabainisha hayo?

Pili,kwanini maulamaa waliokuja baada yake wasiizingatie toba hiyo?

Na hili ni swali muhimu sana nililiuliza katika makala namba  10,lakini hatujasikia jawabu lake!!
Aidha ni kwasababu swali hilo halijaeleweka na watetezi wa Ibnu Sina au halijibiki.
Hebu sasa tuwasikilize maulamaa wengine wanasemaje kuhusu toba ya mzushi kama Ibnu Sina.
Je itatosha kuswali,kusoma Qur'a na pengine mpaka mauti yanamjia msahafu uko kifuani, kuwacha huru watumwa,na kuimba mashairi ya kwamba katubia,je hayo yanatosha?!

Hizi zifuatazo hapa ni baadhi ya kauli za maulamaa;

Amesema Imamu Abu Shaamah,alipokuwa akiupinga wasia ulio nasibishwa na Bwana Mtume rehma na amani zimfikie na kumtaka mwenye wasia huo atubie;

قال الإمام أبو شامة:

" ....وقد قال النبي صلى الله عليه وسلم:

( من قال علي ما لم أقل فليتبوأ مقعده من النار)

وقد قال مفتري هذه الوصية على رسول الله ما لم يقل وكذب عليه كذبا صريحا خطيرا فما أحراه بهذا الوعيد العظيم

وما أحقه به إن لم يبادر بالتوبة وينشر للناس أنه قد كذب هذه الوصية على رسول الله لأن من نشر باطلا بين الناس ونسبه الى الدين

لم تصح توبته منه إلا بإعلانها وإظهارها حتى يعلم الناس رجوعه عن كذبه وتكذيبه لنفسه لقول الله عز وجل

(( إن الذين يكتمون ما أنزلنا من البينات والهدى من بعد ما بيناه للناس في الكتاب أولئك يلعنهم الله ويلعنهم اللاعنون إلا الذين تابوا وأصلحوا وبينوا فاولئك أتوب عليهم وأنا التواب الرحيم))

فأوضح الله سبحانه وتعالى في هذه الآية الكريمة أن من كتم شيئا من الحق لم تصح توبته من ذلك إلا بعد الإصلاح والتبين..))

الباعث فى انكار البدع والحوادث **116/1**.

"….na amesema Mtume rehma na amani zimfikie;
*(mwenye kusema (kunizulia ) yale ambayo sikuyasema,basi na ajichagulie mahala pake motoni).*
na amesema huyu mwenye kumzulia Mtume wasia huu yale ambayo hajayasema,na amemsemea uongo wa wazi,tena wa hatari,anastahiki zaidi kupata adhabu hii,iwapo hakufanya haraka kuleta toba,na kuwatangazia watu kwamba wasia huu amezuliwa Mtume,
Kwasababu mwenye kueneza batili kwa watu na akainasibisha na dini,haitosihi toba yake ila kwa kuitangaza kuidhihirisha mpaka watu wajue kurudi kwake (kuwacha) uongo wake,na aikadhibishe nafsi yake(aseme kwamba yeye ni muongo) kwasababu ya kauli yake Allah;
Akaitaja aya ya 160 ya Surat al Baqarah,kisha akasema;
Ameweka wazi Allah katika aya hii kwamba mwenye kuficha kitu chochote katika haki haitosihi toba yake kwa hilo mpaka atengeneze na abainishe.."

Tazama kitabu chake; al baith fi inkaaril bidai wal hawaadith.1/116.

Swali,je Ibnu Sina amefanya lipi kati ya masharti hayo? Tunaomba jawabu la kielimu kutoka watetezi wa Ibnu Sina.

قال الإمام ابن القيم:

فتوبة هؤلاء الفساق من جهة الإعتقادات الفاسدة بمحض اتباع السنة ولا يكتفى منهم بذلك أيضا حتى يبينوا فساد ما كانوا عليه من البدعة

إذ التوبة من ذنب هي بفعل ضده ولهذا شرط الله تعالى في توبة الكاتمين ما أنزل الله من البينات والهدى البيان لأن ذنبهم لما كان بالكتمان كانت توبتهم منه بالبيان قال الله تعالى:

(( إن الذين يكتمون ما أنزلنا من البينات والهدى من بعد ما بيناه للناس في الكتاب أولئك يلعنهم الله ويلعنهم اللاعنون إلا الذين تابوا وأصلحوا وبينوا فأولئك أتوب عليهم وأنا التواب الرحيم ))

وذنب المبتدع فوق ذنب الكاتم لأن ذاك كتم الحق وهذا كتمه ودعا إلى خلافه فكل مبتدع كاتم ولا ينعكس

مدارج السالكين بين منازل إياك نعبد وإياك نستعين **1/363**.

Amesema Imamu Ibnul Qayyim aliyefariki mwaka 751 h ;

"Na toba ya hawa mafasiki katika upande wa itikadi mbovu ni kwa kufuata Sunna,na wala halitawatosha hilo mpaka wabainishe ubaya wa waliyo kuwa nayo katika Bid'a
Kwasababu toba ya dhambi ni kufanya kinyume chake,na kwasababu hii ameshurutisha Allah katika toba ya mwenye kuficha aliyo yateremsha Allah katika ubainifu na uongofu kubainisha,kwasababu ilipokuwa dhambi yao ni kwa kuficha basi toba yao itakuwa ni kwa kubainisha, kisha akaitaja aya ya 160 ya surat al Baqarah na akasema;

Na dhambi ya mzushi ni zaidi ya dhambi ya mwenye kuficha, kwasababu huyo ameficha haki,na ama huyu ameificha haki,na akalingania kinyume na haki,kwahiyo kila mzushi ni mwenye kuficha,na si kila mwenye kuficha ni mzushi".
Madaarijus saalikin;juz 1, uk 363.
Tumepata faida katika maneno haya ya mwanawachuoni huyu wa Sunna kwamba;

- toba ya mtu mzushi ili ikubalike ni lazima mzushi huyo abainishe uzushi wake huo.

- Toba ya dhambi ni kufanya kinyume chake,je kuswali ni kinyume cha kusema Allah hajui mambo kwa undani? kuacha huru watumwa ni kinyume cha kusema viwiliwili havito fufuliwa? Kuoga nikinyume cha kusema ulimwengu hauna mwanzo? Lakini ujinga na hawaa ya nafsi ni vitu vibaya sana katika dini!

- Dhambi ya mzushi ni zaidi ya dhambi ya mwenye kuficha haki, kwahiyo ikiwa kwa mwenye kuficha ni lazima katika toba yake kubainisha,basi kwa mzushi ni lazima zaidi,

basi ni wapi hapoalipo bainisha Ibnu Sina akastahiki kuadhimishwa? Bado Swali hili linahitaji jawabu.

Amesema Imamu al Qur'tuby aliyefariki mwaka 671 h ;

{ قوله تعالى : { إلا الذين تابوا وأصلحوا وبينوا فأولئك أتوب عليهم وأنا التواب الرحيم

قوله تعالى : { إلا الذين تابوا } استثنى تعالى التائبين الصالحين لأعمالهم وأقوالهم المنيبين لتوبتهم ولا يكفي في التوبة عند علمائنا قول القائل : قد تبت حتى يظهر منه في الثاني خلاف الأول ....."

"Kauli yake Allah;
*{Ila wale ambao wametubu,na wakatengeneza (amali zao) na wakabainisha (yale waliyo yaficha)..."*

Kauli yake; *"ila wale ambao wametubu..."*amewatoa Allah wenye kutubia,wenye kutengeneza matendo yao,kauli zao, na wenye kunyenyekea katika toba zao.
Na wala haitatosha toba mbele za maulamaa wetu kwa kauli ya mwenye kusema (mwenye kutubia) nimetubu, mpaka idhihirike kwake katika hali ya pili kinyume na hali ya kwanza...".

Tafsirul Qurtuby 2/184.

Na amesema Imamu al Jassaas aliye fariki mwaka 370 h;

قوله تعالى : "إلا الذين تابوا وأصلحوا وبيّنوا..." يدل على أن التوبة من الكتمان إنما يكون بإظهار البيان،وأنه لايكتفى فى صحة التوبة بالندم على الكتمان فيما سلف دون البيان فيما استقبل..."تفسير أحكام القرآن 143/1.

"kauli yake Allah;
*{Ila wale ambao wametubu,na wakatengeneza (amali zao) na wakabainisha (yale waliyo yaficha)..."*

Inafahamisha kwamba toba ya kuficha inakuwa kwa kubainisha,na haitotosha katika toba kujuta kwasababu ya kuyaficha yaliyo pita,pasi na kubainisha yajayo..".
Tafsir ah'kamil Qur'an ya al Jassaas 1/143.

Ndugu muislamu hebu yazingatie hayo maneno niliyo yapigia mstari,yasome kwa utulivu,na uyarudie tena, utangundua haya yafuatayo;
-Toba ina masharti yake,ili ikubalike ni lazima masharti hayo yatimie, yasipotimia,toba hiyo haikubaliki.
-Kwa mwenye kuficha ukweli,kutetea batili ni lazima abainishe ukweli huo,na aivunje batili hiyo ndiyo toba itakubaliwa na haitotosha kujuta tu.

-Masharti yote hayo Ibnu Sina hakutimiza hata moja,
ikiwa Ibnu Sina hakutimiza masharti hayo ya toba,

je mnataka toba yake ikubalike kwasababu tu A.M.Y.C. wanamuadhimisha?

Kwa kufupisha maudhui hii ni kwamba mtu yoyote atakaye lingania Bid'a au kufru,au upotevu wa aina yoyote ile,iwapo anataka kutubia ni lazima aibainishe bid'a hiyo kuwa ni bid'a,na kufru hiyo kuwa ni kufru,na upotevu huo kuwa ni upotevu.
Ama kuimba mashairi,au kuswali au kusoma Qur'an au kufanya mengineyo katika amali za kheri,bila ya kubainisha upotevu aliokuwa akiulingania na kuukana,toba hiyo haitokubalika na wala sisi hatuta muhukumu kuwa ametubia.
Na hivi ndivyo maulamaa wa Ah'li Sunna walivyo mchukulia Ibnu Sina.

Pamoja na kwamba Imamu Dhah'by amenukulu kauli ya Ibnu Khallikan inayosema kwamba Ibnu Sina kabla ya kufa kwake alioga akaswali,na akawa anatoa sadaka,na kuwaacha huru watumwa,na kuhitimisha Qur'an kila baada ya siku tatu bado.tunamuona yeye yuko mstari wa mbele akisema;
Si halali kupokea riwaya kutoka kwake !!!
Allah asiwe radhi naye!!!

Kwanini ewe Imamu? na hali yakuwa mtu huyu ametubia? Kwani hujui kwamba toba inabomoa yaliyo pita ?
Kwani hujui kwamba mwenye kutubia dhambi ni kama mtu asiye na dhambi??
Kwani hujui kwamba Allah ni mwingi wa msamaha,mwingi wa huruma?

Maswali yote haya yanatakikana yaelekezwe kwa Imamu Dhah'by,Ibnu Taymiyyah,Ibnul Qayyim,Ibnu Hajar ,Abu Hamid al Ghazaaly,Siddiq Hassan Khan al Qannuwjee,na wengineo katika maulamaa wa zama hizi walio mkufurisha, kama vile Sheikh Abdul Aziz al Rajihi,ambaye ni mmoja katika jopo la kamati ya maulamaa wa Saudi Arabia.

Bila shaka jawabu yao itakuwa kama ifuatavyo,na kama ilivyo tangulia;
-Ni kwamba toba ina mashar'ti yake, yakitimia masharti hayo toba itakubalika,na kama hayakutimia basi toba hiyo si sahihi.
-Na Ibnu Sina hakutimiza masharti ya toba kama ikiwa imesihi kauli ya kwamba katubia bila shaka vitabu vipo, hebu tuelezwe ni wapi Ibnu Sina kabainisha na kuukana upotevu wake?

Amesema Sheikh Salim Barahiyan mudir A.M.Y.C. alipokuwa akizitaja alama za anaowaita Salafiyya Jadida kwa dhulma na uadui;

"Alama ya kwanza;wamebeba fikra za bid'a….wanapenda kukufurisha,wamemuita Sayyid Qutbi zindiki,zindiki alikuwa akiuawa ni kafiri,Ibnu Sina wamemkufurisha! Toba yake hawaitaki maanake wao ndio wanao chagua toba mpaka ile ya matangazo…"

Shuhudia mwenyewe ndugu msomaji maneno machache lakini yamejaa upotoshaji wa haki, uongo! ujinga!kuwazulia watu wasiyo yasema!na hivi ndivyo anavyoipeleka mihadhara yake yote dhidi ya wale wote walio na msimamo wa Salaf Swalih!
Jawaba ya maneno haya ya kijinga ni kama ifuatavyo;

-Ni wapi tumemuita Sayyid Qut'bi kuwa ni zindiki? mimi sikumbuki hilo,ninamuomba alithibitishe hilo kwa ushahidi.
Na nina sema kwamba; kama nimesema hivyo basi namuomba Allah anisemehe, na ninasema wazi kuwa nimekosea,na ninatubu kwa Allah, maana sijafikia kumkufurisha Sayyid Qutbi, wala hakuna mwanawachuoni yoyote wa ki Sunna aliye mkufurisha.

Ama kusema kwamba; Sayyid Qut'bi anakauli za upotevu na bid'a, k.v. kauli ya" wih'datul wujudi" hili limethibitishwa na maulamaa wakubwa kama vile Albany, Ibnu Uthaimin na wengineo, na si Qassim Mafuta kama wanavyodai wajinga wasio fahamu.

Na pamoja na hayo pia maulamaa hawa hawakumkufurisha kwa kutotimia vigezo vya kumkufurisha,nao ni ujinga wake katika dini, kama tutakavyo lieleza hilo katika mahala pake.

-Ama kusema kwamba sisi ndiyo tunao chagua toba za watu, hii ni kauli ambayo haistahiki kusemwa hata na mtu mjinga seuze huyo aitwaye Sheikh na Mudir wa Taasisi.
Na bila shaka ndugu muislamu yamekubainikia maneno ya wanawachuoni wa Ah'li Sunna wal Jamaa k.v.Ibnul Qayyim,al Qur'tuby, Abu Shaamah,Ibnu Uthaimin juu ya toba ya mzushi na mwenye kuitangaza batili na kuitetea.

-Ama madai yake kwamba sisi tuna tabia ya kuwakufurisha watu,kwasababu tunasema Ibnu Sina ni kafiri, huo ni uzushi usio na mfano wake.

## 6- Ufahamu mbaya wa kauli ya Ibnu Khaldun

Jambo la sawa kwa mtu wa Sunna anapojiliwa na haki kwa hoja na dalili kutoka kwa yoyote yule,ni kuifuata haki na kuacha ubishi na ukaidi.

Ndugu zetu hawa baada ya kuwafahamisha ubaya na uovu wa kumuadhimisha Mul'hid huyu (Ibnu Sina) na kwamba hivyo siyo sawa kwa mtazamo wa Sunna.

Badala ya kufuata haki na ukweli wao hawakutaka kuufuata bali wakaanza ubishi na ukaidi na kutafuta dalili za kumtetea Ibnu Sina na kumsifia kwa sifa kemkem na zikakusanywa hoja hata zile zisizo kichwa wala miguu ilimradi tu,awe Ibnu Sina afaa kuadhimishwa!

Kwa mujibu wa maneno ya Sheikh Salim Barahiyan,Mudir A.M.Y.C. ni kwamba Ibnu Sina ametubu,na ameyakana baadhi ya mambo ambayo yalimtia katika ukafiri, kama vile kuitakidi kwamba viwiliwili havito fufuliwa na katika kulithibitisha hilo Mudri huyo akayataja maneno ya Ibnu Sina yaliyonukuliwa na Ibnu Khaldun katika kitabu chake Muqaddima,
lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba Sheikh huyo hakuelewa kwanini Ibnu Khaldun ameyataja maneno hayo,
kwasababu kuwa hawezi kusoma sawasawa, tena mpaka Qur'an pia huisoma makosa!
na anaposoma huwa mara nyingi haelewi au huleta maana tofauti na ilivyo kusudiwa, na mfano wa wazi ni haya maneno ya Ibnu Khaldun.
Labda tuyanukulu maneno hayo ujionee,amesema Ibnu Khaldun;

"...و أما ما وراء ذلك من السعادة التي وعدنا بها الشارع على امتثال ما أمر به من الأعمال و الأخلاق فأمر لا يحيط به مدارك المدركين و قد تنبه لذلك زعيمهم أبو علي ابن سينا فقال في كتاب المبدأ و المعاد ما معناه : إن المعاد الروحاني و أحواله هو مما يتوصل إليه بالبراهين العقلية و المقاييس لأنه على نسبة طبيعية محفوظة و وتيرة واحدة فلنا في البراهين عليه سعة
و أما المعاد الجسماني و أحواله فلا يمكن إدراكه بالبرهان لأنه ليس على نسبة واحدة و قد بسطته لنا الشريعة الحقة المحمدية فلننظر فيها و ليرجع في أحواله إليها".
فهذا العلم كما رأيته غير واف بمقاصدهم التي حوموا عليها مع ما فيه من مخالفة الشرائع...."

"...Ama yaliyo nyuma ya hayo katika katika mambo mema ambayo sheria imetuahidi kwa kuyafuata yale yaliyo amrishwa miongoni mwa amali na tabia,ni jambo ambalo halidirikiwi na akili za wenye utambuzi na ametanabahi hilo kiongozi wao Abu Ally Ibnu Sina akasema katika kitabu chake al mab'dau wal ma'ad kwa maana ya maneno yake;

"hakika kurudishwa (kufufuliwa) roho na hali zake ni katika mambo yanayo fikiwa(kufahamika)kwa akili na vipimo,kwasababu jambo hilo liko katika mnasaba mmoja wa kimaumbile wenye kuhifadhiwa,na mtindo mmoja,kwa hiyo tuna wasaa katika mambo ya kiakili.

Ama kurudishwa(kufufuliwa) viwiliwili na hali zake, haiwezikani kulifahamu hili kwa akili kwasababu hilo haliko katika mnasaba mmoja,na hilo lime kunjuliwa na sheria ya haki ya Muhammad basi na litazamwe huko,na kuerejewa hali zake".
Na elimu hii kama ulivyoiona haitoshelezi makusudio yao ambayo wameyapigia wigo juu yake,pamoja na yale yaliyomo ndani yake katika kuhalifiana na sheria…." mwisho wa kunukulu,tazama Muqaddimatul Ibnil Khaldun uk536-537.

Mudir (Barahiyan) anadai kwamba eti maneno haya ni ishara katika ishara za kwamba Ibnu Sina ametubia na kubainisha batili yake!
Lakini jambo baya zaidi ni kwamba hakujitokeza mtu wa kumhoji kielimu juu ya ibara hizi,bali washabiki wakabaki kupiga Tak'bira za nguvu!!
Ama kweli maradhi ya ujinga ni maradhi mabaya mno!
Lau kama kungekuwepo na mtu aliye na upeo wa kufahamu na kupewa nafasi ya kuhoji angestahiki kuhoji hivi;
-Ni lini Ibnu Sina alitubia?
-Je kitabu hicho alikiandika lini? je kitabu hicho ni katika vile vitabu vya mwanzo au ni katika vya mwisho? maana maulamaa wametubainishia vitabu vyake vya mwanzo na vya mwisho na hiki si katika vitabu vyake vya mwisho!
-Ametubia kwa kusemaje? Kwamba Allah anayajua mambo kwa undani?Au amesema kwamba ulimwengu una mwanzo?
Hapa Ibnu Khaldun haelezei habari za toba ya Ibnu Sina, bali anataka kuthibitisha namna wanafalsafa walivyo filisika,kiasi ambacho wanafikia mahali akili zao zinagonga mwamba,na jambo hili hata kiongozi wao Ibnu Sina ametanabahi na kuligundua,ndiyo akanukulu maneno yake yenye kuishiria hilo! sasa toba hapo iko wapi?
Je ni zipi sharti za toba?
Au sheikh umekusudia kuwatia watu mchanga wa macho?
Na bila shaka aliugundua udhaifu wa hoja zake katika suala hili ndiyo maana akakataa mjadala wa wazi na wa siri!

Mara tunasikia kwamba Ibnu Sina ametubia kwa kuimba mashairi!
Je katika mashairi yenyewe amesemaje?
Je amesema kwamba;
Dunia ina mwanzo?
Allah anajua mambo kwa undani?
Viwiliwili vitafufuliwa?
Au ni nyimbo tu?

Je hayo mashairi aliyoyataja Ibnu Hajar aliyekuja miaka mia nne baada yake ameyanukulu kutoka kitabu gani cha Ibnu Sina? Au kwa sanadi gani sahihi?
Au hilo halikuzingatiwa? Hebu yatazamwe maneno vizuri mtagundua kitu kama mnaelewa!
Na msipoelewa ulizeni,kwasababu kuuliza si ujinga!
- Ama kuhusu jawabu lake juu ya neno" yuqalu"
Sheikh amedhihirisha upeo wa elimu yake ya hadithi,hili mimi sito lijibu nawaachia wale walio ramba japo kidogo ladha ya elimu hii wahukumu,baina ya data feki zilizo tolewa na sheikh huyo,na uhakika wa mambo ulivyo.
Lakini kwanini mpaka mtu afikie kudanganya katika mambo ya kielimu?

## Je ni sawa kuwalinganisha watu waovu na watu wema?

Sheikh Barahiyan katika kumtetea Sheikh wake Ibnu Sina pamoja na ukafiri wake alio kuwa nao akataka kufananiza kati ya mulhid huyo na Sheikhul Islam Ibnu Taymiyyah Allah amrehemu kwa kudai kwamba Ibnu Taimiyyah amezungumza maneno ya kikafiri; (kwamba moto wa akhera utazimika) kisha akahoji kwa ukali;
iko wapi basi toba yake,wapi ametangaza toba hiyo lete lete letee!!!
Sheikh akazungumza kwa kupotosha jambo ambalo mimi nina asilimia kubwa kwamba yeye anafahamu tofauti iliyopo kati ya watu wawili hawa na hali zao.
Na kama hajui basi ni hasara kubwa mno kwa Sheikh kama huyu kutolijua jambo hilo,na pia ni hasara pia kwa wanasunna ambao humfuata yeye kwa kila asemalo.
Jambo lililo nihuzunisha mimi zaidi ni uelewa wa baadhi ya watu kutokana na maelezo ya Sheikh,
ukiwaambia Ibnu Sina hakuleta toba ya dhahiri,wala hakuukana ukafiri wake alio kuwa nao,haraka kabisa wanasema;
mbona hata Ibnu Taimiyyah amekufuru iko wapi toba yake?!
Kwasababu hivyo ndivyo Sheikh alivyowaelewesha watu katika kumtetea Imamu wa makafiri Ibnu Sina.
Hivyo basi,tunahoji kama ifuatavyo;

-Je kwa kauli hiyo ya Ibnu Taimiyyah ni nani katika maulamaa wa Sunna aliyemkufurisha Ibnu Taimiyyah?

-Je ni maulamaa wangapi wa kisunna walio mkufurisha Ibnu Sina kwa itikadi zake?

- Je unajua ni kwanini huyu akufurishwe,na yule asikufurishwe?

Je ni kwasababu ya upendeleo au kwa misingi ya kielimu?

-Je Sheikh anajua kwamba Ibnu Taimiyyah baada ya miaka 30 ya kusema maneno hayo alileta kauli ya kuipinga kauli yake ya kwanza? Aseme sijui ili afahamishwe wala asiwe mkaidi.

Je ni sawa kumfananisha mwanawachuoni ambaye maisha yake yote ameyamaliza katika kuzipigania Sunna za Mtume rehma na amani zimfikie na kuzitetea, na akafa katika hali hiyo,kumfananiza na mtu mzushi, mul'hid, Qurmutwiyu aliyeishi katika kuzitetea fikra potofu za kina Pilato,Erasto,na kumnasibishia Allah ujinga!
Je ni sawa kati ya watu wawili hawa? -

{أَفَنَجْعَلُ الْمُسْلِمِينَ كَالْمُجْرِمِينَ * مَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ } القلم35-36.

*(Je tutawafanya waislamu ni kama waovu(makafiri) mna nini nyinyi vipi mnahuku) al Qalam 35-36.*

Kabla ya kumaliza makala hii niliazimia kuweka mlango maalumu wa kubainisha makosa ya Sheikh ya kisheria,na ya kilugha ambayo mengine yana athiri katika kuleta maana, na hatima yake kupotosha maana sahihi,lakini nikaona kwamba makala itarefuka mno,na hakuna faida kubwa kwa wasomaji.
Lakini hapa nitatoa mfano mmoja miongoni mwa makosa hayo mengi,sheikh anasema kwamba Ibnu Sina amefariki na ugonjwa wa Quwailij

قُوَيلِج

Na huu ni uongo mpevu!! Neno hili halisomwi hivi.
Bali husomwa QUULANJU!!

قُولَنج

Na amelirudia neno hili mara nyingi,na wala hakuna wa kumrekebisha,bali hukosea mpaka aya waziwazi na hakuna wa kumrekebisha!!
Lakini bado nina azma yakuweka makala kamili juu ya suala hili ili wasomaji mjionee wenyewe ! Wallahul Musta'anu.

## *Khatima*

*-Mwisho nina khitimisha makala hii kwa kusema kwamba haifai kuwaadhimisha watu wa Bid'a na hasa wale walio kufurishwa kwasababu ya bid'a zao kama Ibnu Sina.*

*-Ukaidi, ubishi na ubabaishaji katika dini haufai,unapo kosolewa kwa hoja na dalili hakuna budi kuufuata ukweli hata ukidai umesh'tukiziwa na huja nasihiwa !hiyo si hoja ya kukataa haki,na ukweli.*
*-Toba ya mtu wa bid'a,au mtu anayelingania upotevu ni kubainisha bid'a hiyo na upotevu huo,na Ibnu Sina haku fanya hivyo.*
*Jawabu lolote litakalo tolewa tunaomba liwe la kielimu, na lisiwe la hamasa na kejeli.*
*-Bila ya kusahau kuwanasihi ndugu zetu wa Ansaar Muslim Youth Centre Tanga kulifuta jina la shule AVICENNA (Ibn Sina) na kuiitashule hiyo kwa jina lolote linalo kubalika katika sheria,kama majina ya maulamaa wa Ahli Sunna au maswahaba.*
*Kwa faida zaidi fuatilia mfululizo wa makala zetu hizi;*

*-Upambanuzi juu ya hukumu ya picha.*

*-Wajue Maimamu wawili wa Sunna katika zama hizi Rabii al Mad khaly na Muq bil al Waady kwa mtazamo wa maulamaa wa Sunna juu yao na walinganizi wa bid'a (HIZBIYYUN).*

*Ni kina nani Salafiy Jadida?*

*Itikadi za Sayyid Qutbi na Hassan al Banna kwa mtazamo wa sheria.*

*Ikh wanul muslimina katika mizani ya Sunna.*

***Nb;***
***ukiipata makala hii toa copy nyingine ili kueneza ujumbe,Allah atakupa ujira wa kutangaza kheri.***

وبالله التوفيق

وصلى الله وسلم وبارك على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين